**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA

# SHULE YA SEKONDARI MPITIMBI

**S0720**

**JULAI , 2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI**

**YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0757282281/ 0715498635**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0627626850/ 0759330279/ 0750572132**

**Matron: 0687813742/07530311665**

Shule ya Sekondari Mpitimbi
S.L.P 878,
**Songea – Ruvuma.**
18.04.2024

**Kumb: Na. SO/MPSS/JO. I /VOL. 09**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………...**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MPITIMBI HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA MKOA RUVUMA MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024/2025** na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Mpitimbi ipo umbali wa **Kilometa 25** Kusini mwa Mji wa Songea Usafiri wa basi kutoka mjini Songea unapatikana katika kituo cha mabasi Majengo ( Songea mjini) Nauli ni Shilingi elfu tatu (**Tshs 3000/=).**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…………** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………...**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

(i) Sare ya shule hii sketi ni ya rangi ya **karoti (kitambaa namba 1)** na Mwanafunzi anatakiwa awe na sketi mbili. Maelezo ya mshono ni sketi yenye alama ya V mbele kama ya Polisi wa kike iwe ndefu sentimeta 5 toka kwenye kisigino cha miguu

(ii) Shati la shule ni jeupe, mikono mirefu (tetron).

(iii) Kwa wanafunzi wanaovaa Hijabu; Rangi ya hijab (kijuba) ifanane na shati la shule, ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

(iv) Sare ya michezo kwa shule hii ni jezi rangi ya **blue (Adidas)** juu na chini na viatu vya raba

(v) viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

(vi) Soksi jozi tano au zaidi **rangi nyeupe.**

(vii) Sweta la shule rangi ya **chokoleti** nunua masweta mawili

(viii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni ya rangi ya **chokoleti** kitambaa kizito, aje na jozi mbili za (shamba dress) mshono ni solo, gauni liwe refu sentimeta 5 toka kwenye kisigino, mikono mifupi au mirefu yote inaruhusiwa

(ix) Vesti nyeupe ya kuvalia kwa ndani shati la shule

(x) T-shirt 1 rangi ya kijivu isiyo na kola

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
ii. Madaftari 10 counter book (quire 4).
iii. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa Tahasusi ya HGE
iv. Godoro 1 la 2 ½
v. Shuka pair 2 rangi ya blue bahari, Blanketi 1, foronya 1, chandarua 1. Nguo za ndani za kutosha;
vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
vii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
viii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, na fagio aina ya chelewa kwa wote. Fagio (hard broom) HGL, soft broom HGE na mopa HGLi

ix. Saa ya mkononi

x. Tracksuit rangi ya kijivu (nzito) ni lazima iwe pana kwa ajili ya kuvaa wakati wa Prep (usiku wakati wa kusoma)

xi. Begi la kubebea daftari (School bag)

xii. Fedha za matumizi binafsi kiasi chochote

xiii. Taulo, mswaki, sabuni, mafuta, kitenge doti moja (1)

xiv. Lete cheti cha kuzaliwa

xv. Dumu la kuhifadhia maji ya Kunywa la lita tano (05) rangi nyeupe

xvi. Aje na Solata moja Kwa tahadhari ya **UMEME UNAPOKATIKA.**

xvii. Lete result slip ya Kidato cha nne

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango ilipwe kwenye Akaunti Hii:

NAMBA YA AKAUNTI: **61801200139 (NMB)**

JINA LA AKAUNTI: **MPITIMBI SEKONDARI**

## 3. Sheria na Kanuni Muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ✞ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
ii. wizi
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Mwanafunzi harushusiwi kusuka nywele
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT MPITIMBI SECONDARY SCHOOL**

To the Medical Officer
................................................
................................................
................................................
**Name of Student: ...................................................**
Please examine the above-named student to her/his fitness to pursue secondary education course.

.........................................
PATRICK MATEMBO
**THE HEADMASTER**

1. Eyes ...........................................................................................
2. Ears ...........................................................................................
3. Mouth ..........................................................................................
4. Heart ..........................................................................  ..........
5. Abdomen .......................................................................................
6. Blood ..........................................................................................
7. Urine ..........................................................................................
8. Sputum .........................................................................................
9. Hb ..............................................................................................
10. Leucocytes ...................................................................................
11. E.S.R ..........................................................................................
12. Pregnancy .....................................................................................

Date: .......................................... Signature: .......................................
**MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by the Medical Officer)**
I have examined the above named and consider that he/she is mentally and physically fit/ Not mentally and physical fit for studies.
Signature: .............................. Date: ..........................
Designation: ........................... Station ........................

**JINA LA MWANAFUNZI ............................................................................**

**KIDATO CHA ..................................... TAHASUSI YA .......................................**

**NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao hii itasaidia kutoa taarifa endapo tatizo litatokea. Hatutaki majina ya Ndugu bandia. Tunaomba mzingatie hilo kwa ajili ya usalama wa mtoto wako

| |
|---|
| *Picha ya Mama/Mlezi (Passport size)* |

1. (a) Jina ...............................................................
   (b) Uhusiano .......................................................
   (c) Anuani ..........................................................
   (d) Namba ya simu ...............................................

| |
|---|
| *Picha ya Baba/Mlezi (Passport size)* |

2. (a) Jina ...............................................................
   (b) Uhusiano .......................................................
   (c) Anuani ..........................................................
   (d) Namba ya simu ..............................................

| |
|---|
| *Picha ya Ndugu (Passport size)* |

3. (a) Jina ……………………………………………………
   (b) Uhusiano .......................................................
   (c) Anuani ..........................................................
   (d) Namba ya simu ..............................................

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ...................................................

Tarehe ..........................................................................

| |
|---|
| *Picha ya Mzazi/Mlezi (Passport size* |

**AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU**

Mimi .................................................................... nakubali nafasi niliyopata katika shule ya SEKONDARI MPITIMBI kuendelea na masomo. Ninafahamu kuwa wazazi wangu ndio watakaogharamia masomo yangu, nahaidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na nitakuwa mwanafunzi mwaminifu katika kutimiza na kufuata sheria za shule na kushirikiana na wenzangu katika shughuli zote za shule.

| |
|---|
| *Picha ya Mwanafunzi (Passport size)* |

..............................

**Sahihi ya Mwanafunzi**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ................................................................... nimesoma yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampa mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua zote zinazomhusu mtoto wangu, nitalipa karo ya shule na michango yote inayotakiwa kwa wakati wake.

Barua na ripoti zinazomhusu mtoto wangu zitaletwa kwangu kwa anwani hii
S.L.P .......................................................................
Jina na sahii ya Mzazi/Mlezi ...........................................
Tarehe ......................................................................
Namba ya simu ...........................................................

## FOMU NA. 3: KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI A. MWANAFUNZI

1. Jina kamili (Matatu) .........................................................................
2. Shule ya O-level aliyosoma ....................................................................
3. Namba ya mtihani ..............................................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa ............................................................................
5. Nakubali nafasi niliyopewa/sitaki apewe mwingine (Kata lisilohusika)
6. Naahidi kutomiliki simu shuleni, kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai kama ilivyo ainishwa katika sheria za shule.
7. Sahihi ..........................................................................................

**B. MZAZI/MLEZI**

- Nakubali mwanafunzi apate Elimu yake hapo Mpitimbi Sekondari
- Na kwamba atafuata sheria na maelekezo yote. Vinginevyo aadhibiwe
- Na kwamba mwanafunzi alelewe katika dini ya ..........................................
- Sitampa simu mimi binafsi na Ndugu wote wala kuafiki yeye kuwa nayo
- Na kwamba nitatekeleza masharti/mahitaji yote yaliyoainishwa.
- Na kwamba nitalipa michango yote kwa wakati bila usumbufu wowote.
- Na kwamba sitomhamisha mwanangu bila sababu ya msingi

Jina la Mzazi/Mlezi ................................. Namba za simu ........................ Anuani .................................. Kijiji/Mtaa ...................................... Sahihi ya Mzazi/Mlezi .............................................. tarehe ...........................................

...................

**PATRICK P. MATEMBO**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MPITIMBI
S. L. P. 878 SONGEA.

**FOMU NA. 4: TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (IJAZWE NA MWANAFUNZI)**

Jina la Mwanafunzi: (Matatu) .......................................................................................... Tarehe ya kuzaliwa ..........................................................................................
Jinsia ..........................................................................................
Umri ..........................................................................................
Nyumba (Kitongoji) ...................................... Wilaya ................... Mkoa ....................
Simu ya Mzazi/Mlezi ..........................................................................................
Jina la Baba/Mlezi .................................... Uhusiano .................. Yupo hai? ................
Jina la Mama/Mlezi ................................. Uhusiano .................... Yupo hai? ................
Anuani yake ..........................................................................................
Kazi ya Mzazi/Mlezi ..........................................................................................
Umechaguliwa kuingia kidato cha tano/mchepuo/Tahasusi .............................................
Shule uliyotoka .............................. Ipo Wilaya ya .................... Mkoa ........................
Tarehe ya kuripoti Mpitimbi shuleni ........................................................................
Ndugu yako wa karibu aliyopo

1. Songea Mjini ni (Jina) ..........................................................................
   Uhusiano naye ..........................................................................
   Anuani yake ................................................. Simu na ....................................
2. Mbinga Mjini ni (Jina) ..........................................................................
   Uhusiano naye ..........................................................................
   Anuani yake ............................................. Simu na. .......................................
3. Mahali pengine ndani ya Mkoa wa Ruvuma (Tunduru, Nyasa, Mbinga Dc, Madaba, Namtumbo)
   Jina ..................................................... Namba ya simu .................................
   Uhusiano .............................................

Mimi .............................................................. nakiri kwamba taarifa nilizotoa ni sahihi
Sahihi ............................................................. tarehe ...........................................

**NB: ENDAPO MWANAFUNZI ATATOA TAARIFA ZISIZOSAHIHI ATACHUKULIWA HATUA ZA KINIDHAMU**

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....................

**PATRICK P. MATEMBO**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MPITIMBI
S. L. P. 878 SONGEA.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0757282281/ 0715498635**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0627626850/ 0759330279/ 0750572132**
- **Mwandamizi Taaluma 0658376735**
- **Mwandamizi Malezi 0757115381**
- **Matron: 0687813742/ 0753031665**

## FOMU NA. 6: IMPORTANTS AND ESSENTIAL REFERENCES

Vitabu hivi ni muhimu unashauriwa uwe navyo:-

**A. HISTORY**

1. Major issue in Africa History ICD
2. Major events in Africa History MWIJAGE
3. The Political economy Imperialism BY NABUDERE
4. Africa since 1800 4 edition BY ROLAND OLIVER ATMORE
5. The making of modern Africa Vol. 1
6. How Europe under developed Africa WALTER RODNEY
7. The 20 century by Duff M.N
8. Europe from 1815 by Peacock

**B. GEOGRAPHY**

1. Certificate of geography (Oxford from 3 by (1) Mary Mugo (2) Robert Karuggah (3) Paul Kibuuka
2. General Geography in diagrams RB Bunner
3. Regional Geography By Nyangwine/Msabila
4. Photography Interpretation and elementary Surveying for secondary level new edition 5. Integrate geography approach, human activities Julian Sima

**BY S.E. DURA**

6. Certificate Human and Economic Geography By Morgans and Leong chang
7. Principles in physical Geography By Monkhouse
8. Geography an integrate approach 2nd ed By david Waugh (2009)

**C. ENGLISH LANGUAGE PAPER 1**

1. A COMPLETE English course for form six MICHAEL KADEGE
2. English for form five and six MICHAEL KADEGE
3. Teaching English as a foreign language G. Broughton, et al
4. Longman English Grammar L.G Alexander
5. Advanced learners Dictionary OXFORD

**PAPER III 1. NOVIES**

- (a) The beautiful one not yet born A.K. AMAH
- (b) A grain of wheat NGUNGI WATHIONGO
- (c) A man of the people CHINUA ACHEBE
- (d) Vanishing shadows N. KAYOMBO

**2. POETRY**

- (a) Selected poems form Institute of Education
- (b) Appreciation of poetry form 5 and 6
- (c) Comprehensive analysis of literary works novel and short stories
- (d) Analysis and interpretation of literary works plays and introduction to literature

**(i) BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. K. Respicus & M. Lugano (2010) Basic and Applied mathematics (BAM), Nyamabari Nyangawine Publishers Dar – Tanzania.

2. C.J. Trauter: Advance level pure mathematics.
3. Backhouse: pure mathematics 1 & 2
4. L. Bostock: Further pure mathematics.
5. Mathematics for class XI, S. CHANDS (2015).

**D. ECONOMICS**

1. Modern Economics by mudida
2. Managenal economics by oxford
3. Micro Economics by Meconnel

**E. GENERAL STUDIES**

(i) General studies for level Certificate form V BY RICHARD MBALASE
(ii) General studies for A'level certificate from vi BY RICHARD R. MBALASE

Viambatanisho vya rangi sketi na mshono wake pamoja na sweta la shule



Sweta la shule rangi ya chocolate



Sketi ya shule rangi ya karoti